ISSN 0856 - 034X

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA

Supplement No. 18 ***1st May, 2020***

SUBSIDIARY LEGISLATION

to the Gazette of the United Republic of Tanzania No.18. Vol.101 dated 1 May, 2020
Printed by the Government Printer, Dodoma by Order of Government

TANGAZO LA SERIKALI NA. 304 limetolewa 1/5/2020

SHERIA YA UGAVI WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA,

(SURA NA. 272)

(Imetolewa kwa mujibu wa Kifungu Na.28 (d))

AMRI YA MAMLAKA YA UGAVI WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA TUNDURU ("TUNDURU WSSA"), MAREKEBISHO YA BEI ZA HUDUMA ZA UGAVI WA MAJI NA USAFI WA MAZINGIRA), 2020

Kichwa cha Jina

1. Amri hii itajulikana kama, Amri ya Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira Tunduru ("Tunduru WSSA"), (ya Kurekebisha Bei za Huduma za Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira), ya Mwaka 2020.

Bei na Tozo

2. Bei za majisafi na usafi wa mazingira za Tunduru WSSA zinarekebishwa kwa kuzingatia Jedwali la Kwanza.

Masharti

3. Bei zilizoidhinishwa zitaambatana na masharti yafuatayo:

Gazeti la Serikali Namba 193 la

(a) ifikapo au kabla tarehe 31 Mei 2020, Tunduru WSSA itawasilisha EWURA Mpango wake wa Kibiashara (2019/20-2021/22) uliopitiwa upya

mwaka 2010.

kwa kuzingatia bei zilizoidhinishwa na mpango wa utekelezaji wa masharti ya Agizo hili;

(b) Tunduru WSSA, kwa kutumia mapato yatokanayo na bei zilizoidhinishwa, itatekeleza miradi iliyoainishwa katika Jedwali la Pili;

(c) Tunduru WSSA itafikia viashiria vya utendaji kama ilivyooneshwa kwenye Jedwali la Tatu.;

(d) Tunduru WSSA itatekeleza kifungu cha 43 cha Sheria ya EWURA na kanuni ya sita (6) ya EWURA ya Taratibu za Kukusanya Ada na Tozo;

(e) ifikipo tarehe 30 Aprili 2020 au kabla, Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira Tunduru iwasilishe EWURA vielelezo kwamba ilitoa taarifa kwa wateja wake kuhusu bei mpya za huduma zake na pia ilitoa elimu kikamilifu kwa umma kuhusu utekelezaji wa bei mpya, ikiwa ni pamoja Serikali na wawakilishi wa dini na wa wananchi, katika maeneo yao ya huduma;

Sura ya 418

(f) Tunduru WSSA itahakikisha ripoti zake za kifedha zinakaguliwa na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG) au taasisi yeyote ya ukaguzi wa fedha iliyoidhinishwa kama kifungu cha 33 (1) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma na kupeleka nakala za taarifa za kifedha zilizokaguliwa kwa EWURA;

(g) Tunduru WSSA itahakikisha maji yanayopelekwa kwa wateja ni safi na salama;

(h) kabla ya Tarehe 30 Juni, 2022 Tunduru WSSA itahakikisha inapata eneo la ardhi kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya kutibu majitaka;

(i) Tunduru WSSA, kwa kila mwaka kama sehemu ya taarifa yake ya utendaji ya mwaka, itawasilisha taarifa ya utekelezaji wa masharti yaliyopo kwenye Agizo la Bei na kila kifungu cha gharama katika mahitaji ya fedha yaliyoidhinishwa kama yalivyoainishwa katika Jedwali la Nne; na

(j) Tunduru WSSA itaendelea kuwasilisha EWURA taarifa zake za fedha na utendaji kwa mujibu wa matakwa ya EWURA. Taarifa hizi zitatumiwa na EWURA katika kufanya tathmini ya utendaji wa Tunduru WSSA ikilinganishwa na Mamlaka nyingine za Ugavi wa Maji na Usafi wa Mazingira na uboreshaji wa huduma zake. Pia EWURA itazingatia tathmini hii katika kufanya maamuzi ya maombi yote yatakayowasilishwa na Tunduru WSSA katika siku zijazo.

Kusitisha matumizi ya Agizo la Bei Na. 11-014 la tarehe 1 Juni 2011

4. Amri hii inasitisha matumizi ya Amri (Marekebisho ya Bei) Na. 11-014 la tarehe 1 Juni, 2011 katika eneo linalohudumiwa na Mamlaka ya Ugavi wa Maji na Usafi wa MazingiraTunduru ("Tunduru WSSA").

Tangazo la Serikali Na. 304 (linaendelea)

MAJEDWALI

JEDWALI LA KWANZA

(Limetengenezwa chini ya aya ya 3)

BEI, ADA NA TOZO ZILIZOIDHINISHWA

Jedwali 1.1: Bei za Maji za Sasa na Zilizoidhinishwa kwa Wateja Wenye Dira (Shilingi/ Mita ya Ujazo)

Kundi la Wateja	**Bei ya Sasa**	**Bei Zilizoidhinishwa**		
	2018/19	**2019/20**	**2020/21**	**2021/22**
Majumbani				
Daraja 1 (0-5m3)	540	780	850	1,100
Daraja2 (6-10m3)	585	850	930	1,230
Daraja3 (>11m3)	625	910	1,050	1,260
Taasisi	550	820	1,120	1,310
Biashara	605	900	1,200	1,340
Viwanda	760	1,130	1,250	1,350
Magati	1000	1,000	1,000	1,000
Wastani	**613**	**886**	**1,028**	**1,248**

Jedwali 1.2: Bei ya Maji Sasa na Iliyoidhinishwa kwa Wateja Wasio na Dira (Shilingi/Mwezi)

Kundi la Wateja	Bei ya Sasa	Bei Zilizoidhinishwa		
	2018/19	Novemba 2019 hadi Februari 2020	2020/21	2021/22
Majumbani	4,500	4,500	Bei Hazijaidhinishwa	
Taasisi	16,500	16,500		
Biashara	16,500	16,500		
Viwanda	16,500	16,500		

Jedwali 1.3: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Maunganisho Mapya (Shilingi/Unganisho)

Kundi la Wateja	**Ada ya Sasa**	**Ada Zilizoidhinishwa**		
	2018/19	**2019/20**	**2020/21**	**2021/22**
Majumbani	13,500	Asilimia 20 ya Gharama za Maunganisho kama ilivyoelezwa katika Kanuni za Maji za Mwaka 2013		
Taasisi	13,500			
Biashara	13,500			
Viwanda	13,500			
Magati	13,500			

Jedwali 1.4: Ada ya Sasa na Iliyoidhinishwa ya Marejesho ya Huduma ya Maji Baada ya Kukatiwa (Shilingi/Marejesho)

Kundi la Wateja	**Ada ya Sasa**	**Ada Zilizoidhinishwa**		
	2018/19	**2019/20**	**2020/21**	**2021/22**
Majumbani	13,000	15,000	15,000	15,000
Taasisi	13,000	15,000	15,000	15,000
Biashara	13,000	15,000	15,000	15,000
Viwanda	13,000	15,000	15,000	15,000
Magati	13,000	15,000	15,000	15,000

_____

JEDWALI LA PILI

_____

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(b))

MIRADI ITAKAYOTOKELEZWA

Maelezo ya shughuli	Shilingi Milioni		
	2019/20	2020/21	2021/22
Ukarabati na Mabadilisho			
Kununua dira za maji 2,300 kwa ajili ya kubadilisha na kuwafungia wateja wapya	70.00	70.00	100.00
Jumla	70.00	70.00	100.00
Uwekezaji Mpya			
Kujenga bomba la maji (OD11OHDPE)kuelekea maeneo ya Kalanje na Tuleane	-	66.70	132.40
Kujenga bomba la maji kuelekea maeneo ya Ujenzi and Lambai	10.00	20.00	138.20
Kununua pikipiki 2 kwa ajili ya shughuli za kila siku	2.00		5.50
Kununua pikipiki moja ya miguu mitatu	-	-	5.00
Kununua mashine ya kuungia mabomba (portable Butt Fussion machine)	-	3.50	3.50
Jumla (Uwekezaji Mpya)	12.00	90.20	284.60
Jumla ya Gharama za Uwekezaji	82.00	160.20	384.60

JEDWALI LA TATU

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(c))

VIASHIRIA VYA UTENDAJI (2019/20 – 2021/22)

Maelezo	Kipimo	Lengo la Utendaji		
		2019/20	2020/21	2021/22
Idadi ya wateja wapya wa maji safi	Na	100	150	200
Kiwango cha upotevu wa maji	%	20	20	20
Wateja wenye Dira	%	92	100	100
Kiwango cha ufanisi katika ukusanyaji wa mapato	%	90	90	95

JEDWALI LA NNE

(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(i))

MAHITAJI YA FEDHA YALIYOIDHINISHWA (SHILINGI MILIONI)

GHARAMA	Mapendekezo			Marekebisho		
	2019/20	2020/21	2021/22	2019/20	2020/21	2021/22
Uzalishaji wa Maji	98.20	103.00	107.00	98.20	103.00	107.00
Usambazaji	97.00	102.00	107.00	97.00	102.00	107.00
Uondoaji Majitaka	-	-	-	-	-	-
Matengenezo	68.00	79.00	98.00	68.00	79.00	98.00
Watumishi	79.00	93.00	111.00	77.00	92.00	111.00
Utawala	78.45	90.10	98.53	50.95	58.40	66.18
Matangazo	-	-	-	-	-	-
Matukio	6.69	8.23	8.26	6.69	8.23	8.26
Benki	-	-	-	-	-	-
Jumla (Uendeshaji na Matengenezo	427.34	475.33	529.79	397.84	442.63	497.44
Uchakavu	170.00	165.00	165.00	33.96	33.96	33.96
Uwekezaji	-	-	-	82.00	160.20	384.60
Jumla ya Mahitaji ya Fedha	597.34	640.33	694.79	513.80	636.79	916.00
Ondoa: Mapato Mengine	35.00	45.00	50.00	11.90	15.37	17.40
Jumla ya Mahitaji ya Fedha Kutokana na Mauzo ya Maji	562.34	595.33	644.79	501.90	621.41	898.60

Dodoma,
21 Aprili, 2020

NZINYANGWA E. MCHANY,
Mkurugenzi Mkuu